# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA TATU

**13 MEI, 2025**

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA ISHIRINI NA TATU – TAREHE 13 MEI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**289 MHESHIMIWA HASSAN SELEMANI MTENGA (MTWARA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali imefikia wapi kufuatilia kesi inayomkabili *Human Resources Manager* wa Kampuni ya Dangote *Cement* Mtwara.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**290 MHESHIMIWA DKT. ALFRED JAMES KIMEA (KOROGWE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itazipandisha hadhi Sekondari za Ngombezi, Joel Bendera na Kwamndolwa - Korogwe TC kuwa za Kidato cha Tano na Sita.

**291 MHESHIMIWA KABULA ENOCK SHITOBELA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, sababu zipi zinapelekea Mikopo ya Wanawake kuchelewa kutolewa kwa waliokidhi vigezo vyote hasa Wanawake wa Mkoa wa Mwanza.

**292 MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya cha kimkakati kwenye Kata ya Lukozi - Lushoto.

**293 MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KASSINGE (KILWA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka gari la kubeba Wagonjwa katika Kituo cha Afya Nanjilinji Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**294 MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, lini Serikali itawalipa Watumishi Wastaafu waliopandishwa madaraja kisha hatua hizo kusitishwa.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**295 MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, ni hatua gani imefikiwa katika kutekeleza Taarifa ya Wataalam kuhusu Ziwa Tlawi.

**WIZARA YA NISHATI:**

**296 MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, kuna mkakati gani wa kuunganisha gesi kwa ajili ya kupikia kwa Taasisi na Nyumba za Wananchi Mkoani Mtwara.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**297 MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (VWAWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, upi mkakati wa Serikali wa kujenga minara ya simu kwenye Kata ya Ipunga, Nyimbili na Isalalo ili kuboresha mawasiliano.

**WIZARA YA UJENZI:**

**298 MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Kivuko cha Abiria kutoka Kakukuru kwenda Gana - Ukerewe kitaanza kujengwa.

**WIZARA YA FEDHA:**

**299 MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali imewezesha miradi mingapi kwa utaratibu wa ubia wa Serikali na Sekta Binafsi.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**300 MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, kuna mpango gani wa kuwawezesha Wavuvi wa Kigamboni kwa kuwapatia vifaa vya kisasa vya uvuvi.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**301 MHESHIMIWA AMINA ALI MZEE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kuna mpango gani wa kujumuisha Mada ya Ukatili wa Kijinsia kwenye Masomo kuanzia Shule za Msingi nchini.

**WIZARA YA MAJI:**

**302 MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR (NYANG'HWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, kuna mpango gani wa kusambaza maji Kata za Kaboha, Shabaka, Nyang'hwale, Nyaburanda, Mwingiro, Nyugwa ili kumaliza tatizo la maji.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**303 MHESHIMIWA NICODEMAS HENRY MAGANGA (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwagawia Wananchi sehemu ya eneo la Pori la Kigosi ili litumike kwa shughuli za kiuchumi.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA**<br>**13 MEI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD**<br>**KATIBU WA BUNGE**